



Wakati wowote rangi ya risasi hupatikana katika nyumba na majengo yaliyojengwa kabla ya 1978, rangi nyingi za risasi hupatikana katika nyumba zilizojengwa kabla ya 1950. Rangi ya risasi/lead iliyomenyewa au iliyokatwa vipande vipande inaweza kuwa hatari. Maeneo ambapo rangi ya risasi inajipakaa, kama vile fremu za milango, madirisha, au hata sakafu unayotembelea, panaweza kuzalisha vumbi ya risasi/lead. Vumbi ya risasi/lead inaweza pia kutoka kwenye matengenezo ya nyumbani na ukarabati. Ukisiriba mchanga, kukwaruza rangi au kuvuruga rangi ya risasi/lead unaweza kufanya vumbi ya risasi/lead.

Iwapo Unaishi Katika Jengo la Kale au kama umesiriba mchanga ao umedodosa rangi ya risasi/lead

Fuata maagizo haya ili nyumba yako isafishwe kwa kina kuondoa vumbi ya risasi/lead. Ukimaliza kusafisha kwa njia hii, safisha sakafu yako, fremu za chini ya madirisha, miimo ya milango na kitambaa kutoa uchafu au kukoropa mara moja kwa wiki.

Hatua ya 1: Jiandae kabla ya kusafisha.

Angalia ndani ya chumba, vaa glavu na kuchukua vibanzi vya rangi vyovyote vilivyo sakafuni au karibu na madirisha. Kitambaa cha uchafu, taulo ya karatasi, au tishu za kupanguza mtoto hunaweza kukusaidia kuchukua vibanzi hivi. Tupa mbali vibanzi na vitambaa vichafu ndani ya mfuko wa plastiki. Tumia mashini inayoondosha vumbi kwenye sakafu. Mashini zenye vichujio vya HEPA hufanya kazi vizuri. Mashini zenye mifuko ya "Allergen" ni chaguo bora ikiwa hauna mashini inayoondosha vumbi ya HEPA. Usitumie mifagio maana hii itasambaza vumbi ya risasi/lead pande zote.

Hatua ya 2: Changanya maji yako ya kusafisha.

Jaza ndoo ya kusafisha nusu kamili na maji vuguvugu. Changanya na sabuni ya kaya, ukifuata maagizo yaliyo kwenye chupa.



Hatua ya 3: Osha mbao pamoja na sakafu.

Anza na kuosha mbao zilizo karibu ya madirisha, milango na bodi za msingi na vitambaa vyevu kwa maji ya kusafisha. Hakikisha utumike kuanzia juu mpaka chini. Kama kitambaa kinakuwa kichafu, kitupe mbali. Badilisha maji wakati yanageuka chafu. Bwaga maji chafu ndani ya choo.



Hatua ya 4: Osha sakafu.

Ukitumia mchanganyiko mpya wa maji ya kuosha, osha sakafu kwa kikoropesho au kitambaa safi. Unapomaliza, tupa vitambaa vya kuosha, bwaga maji chafu ndani ya choo.



Hatua ya 5: Suuza na kusafisha.

Jaza ndoo na maji. Zamisha vitambaa safi vya kusafisha ndani ya maji na upanguze mbao zote ulizoosha. Ukitumia maji mapya ya kusuuza, koropa au panguza sakafu. Unapomaliza, bwaga maji ya kusuuza ndani ya choo pia usafishe kikoropesho na ndoo. Tupa kando glovu, vitambaa vya kusafisha, pia weka mfuko wa taka katika takataka.

Linda familia yako.

- Angalia kwenye mtandao: maine.gov/healthyhomes
- Ita kwa kutaka shauri : **866-292-3474 • TTY: Ita Maine Relay 711**

